Kwa wazazi wanaotumia huduma zinazofadhiliwa na IRCC

MAELEZO YOTE KUHUSU KUWAHUDUMIA WATOTO WAGENI (CARE FOR NEWCOMER CHILDREN – CNC)

Karibu! Mpango wetu wa CNC umeundwa kuwasaidia watoto ambao ni wageni nchini Kanada na familia zao wanapokuwa wakifikia huduma zinazofadhiliwa na IRCC. Tuko hapa kusaidia.

Tunajua kwamba hiki ni kipindi chenye mabadiliko mengi kwako na familia yako. Lengo letu ni kwa mtoto wako kuhisi amekaribishwa, salama, ilhali tukiunga mkono ukuaji wake na kuendeleza kujiamini kwake familia yako inapokuwa ikitulia nchini Kanada.

WAKATI MTOTO YUPO KATIKA MPANGO WA CNC, LAZIMA WAZAZI WABAKIE KITUONI NYAKATI ZOTE.

Hakuna kitu cha maana kama usalama wa mtoto wako!

Unaweza kuwa na uhakika kwamba wahudumu wetu wamehitimu na wana uzoefu.

- Wahudumu wote wamefanyiwa uchunguzi wa usuli/rekodi ya uhalifu na wamepitia mafunzo ya huduma ya kwanza.
- Tunafuata Masharti ya CNC na tunasimamiwa ili kuhakikisha kwamba tunatimiza viwango vya afya na usalama.
- Ili kuhakikisha watoto wote wanashughulikiwa kwa usawa na kwa heshima, tuna sera ya kusimamia tabia. Lazima wahudumu waimarishe tabia kwa njia nzuri. Kuwaadhibu watoto kimwili au kuongea nao kwa ukali hakuruhusiwi; wala utelekezaji au kutowasimamia.
- Wahudumu wana jukumu la kitaalam na majukumu ya kisheria kuripoti hali yoyote ambayo mtoto ameumizwa au kutelekezwa kwa mamlaka husika.

Jihisi huru kuomba nakala ya sera yetu ya kusimamia tabia au sera ya dhuluma/utelekezaji unaoshukiwa wa watoto iwapo unataka kujua mengi.

Je, unaweza kutarajia nini kutoka kwa CNC?

Jinsi ambavyo tunawatunza watoto kwa kuwaweka katika vikundi nchini Kanada inaweza kuwa tofauti na wa nchi yako. Ikiwa una maswali kuhusu nidhamu, chakula, lugha, elimu au ratiba, tafadhali uliza. Utafiti unaonyesha kwamba watoto hujifunza kupitia kucheza, kwa hivyo wahudumu hupanga shughuli za kielimu na za kucheza za masomo ili kuweza kuendana na mapendeleo, umri, uwezo na tamaduni za watoto. Mtoto wako atajifunza kutangamana na watoto wengine na kukuza ujuzi ambao utamwandaa kwa shule.

Unawezaje kumsaidia mtoto wako kuzoea CNC?

Ni kawaida kwa mtoto wako kuwa na wasiwasi kuhusu kuanza CNC. Wahudumu watakushirikisha ili kufanya mabadiliko haya kuwa rahisi, lakini kwanza, huenda mtoto wako akalia, akakung'ang'aniakwamilia, au kuonyesha tabia nyingine. Kwa mawazo kuhusu jinsi unaweza kusaidia kurahisisha hofu ya mtoto wako, omba nakala ya *Karibu kwenye CNC: Mwongozo wa Wazazi wa Utenganisho wa Polepole*.

Mawasiliano kati ya wazazi na wahudumu ni muhimu!

Tunakuhimiza uweze kuwafahamu wahudumu wetu wa CNC na ushiriki maelezo kuhusu mtoto wako. Wakati sisi wote tunapofanya kazi kwa pamoja, tunaweza kumsaidia mtoto wako vizuri zaidi na kumweka salama.

Funded by: Immigration, Refugees and Citizenship Canada / Financé par : Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada

MAELEZO YOTE KUHUSU KUWAHUDUMIA WATOTO WAGENI (CARE FOR NEWCOMER CHILDREN – CNC)

Hakikisha umewaelezea wahudumu kuhusu:

- mizio au vikwazo vya chakula;
- magonjwa au dawa ambazo mtoto wako anatumia (tafadhali kumbuka: dawa hupeanwa katika hali zinazotishia maisha tu na hazipaswi kuachwa na mtoto mtoto wako au kwenye begi lake);
- na mahitaji au changamoto zozote maalum. Wanaweza kusaidia!

Pia inaweza kuwa muhimu kuwaeleza wahudumu:

- ratiba ya kulala au lishe ya mtoto wako;
- mapendekeo na vyakula ambavyo mtoto wako anavipenda;
- maneno ambayo yanaweza kuwasaidia wahudumu kuwasiliana na mtoto wako;
- maelezo kuhusu familia na ndugu (au leta picha ya familia);
- na njia maalum unazomtunza mtoto wako na unachoweza kutaka kutoka kwa CNC.

Mambo mengine ya kuzingatia:

- Kwa usalama wa mtoto wako, mzazi ambaye amesajiliwa pekee kwenye huduma ndiye anaweza kumleta na kumchukua mtoto wake.
- Lazima kila wakati umwandikishe mtoto wako akiingia na akitoka.
- Mvishe mtoto wako vizuri kwa hali zote za hewa na shughuli atakazokuwa akizifanya kwenye mpango. Ikiwa una maswali kuhusu nini mtoto wako anapaswa kuvaa, uliza wahudumu.
- Ni muhimu kumleta mtoto wako mara kwa mara ili kudumisha ratiba yake na kumwandaa kwa ajili ya shule. Ikiwa ni lazima mtoto wako asiende shuleni, wafahamishe wahudumu.
- Ikiwa mtoto wako ni mgonjwa, mweke nyumbani ili kuzuia kusambaza ugonjwa. Watoto wenye homa au kuhara lazima wasiwe na dalili zozote kwa saa 24 kabla ya kurejea CNC.

MAELEZO YOTE KUHUSU MPANGO WETU WA CNC

Majina ya Watoa huduma: _____
Caregiver's Name / Nom du dispensateur de soins

Saa za CNS: _____
CNC Hours / Heures de garde d'enfant

	Ndiyo Yes / Oui	Hapana Non / Non
Chanjo inayohitajika Immunization required / L'enfant doit avoir été vacciné	◯	◯
Tunatoa vitafunio We provide snacks / Nous fournissons des collations	◯	◯
Beba chakula cha mchana/vitafunio vya mtoto wako Bring food for your child's lunch/snack / Apportez le déjeuner/la collation de votre enfant	◯	◯
Utamhudumia mtoto wako wakati wa chakula cha mchana You care for your child at lunch / Vous prenez soin de votre enfant au déjeuner	◯	◯
Tuna muda wa kulala We have a naptime / Notre programme prévoit une sieste	◯	◯

	Ndiyo Yes / Oui	Hapana Non / Non
Leta sesere ya kuchezea Bring a comfort toy / Apportez un jouet réconfortant	◯	◯
Leta nguo za ziada Bring extra clothes / Apportez des vêtements supplémentaires	◯	◯
Leta viatu vya kuvaa akiwa ndani Bring indoor shoes / Apporter des chaussures d'intérieur	◯	◯
Leta blanketi (ikiwa inahitajika) Bring a blanket (if needed) / Apportez une couverture (si nécessaire)	◯	◯
Leta nepi (ikiwa zinahitajika) Bring diapers (if needed) / Apportez des couches (si nécessaire)	◯	◯

CMAS

KUUNGA MKONO HUDUMA NA MAKAZI YA WATOTO WADOGO WAHAMIAJI

Kwa rasilimali zaidi za wazazi, tembelea: www.cmascanada.ca

Care for Newcomer Children

Funded by: Immigration, Refugees and Citizenship Canada / Financé par : Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada